



MAMLAKA YA KUZUIA RUSHWA NA UHUFUMU WA UCHUMI ZANZIBAR

ZAECA yakutana na Waandishi wa habari Pemba, mapambano dhidi ya rushwa na uhujumu uchumi Zanzibar.

Waandishi wa habari kisiwani Pemba wameombwa kuwa wadau muhimu katika mapambano dhidi ya vitendo vya rushwa na uhujumu uchumi nchini.

Akizungumza na waandishi wa habari huko Gombani Pemba Mkurugenzi wa mamlaka ya kuzuia rushwa na uhujumu uchumi Zanzibar (ZAECA) Ahmed Khamis Makarani, amesema mapambo dhidi ya vitendo vya rushwa na uhujumu uchumi yanahitaji umoja na mashirikiano, hivyo basi amewaomba waandishi wa habari kisiwani humo kuunga mkono juhudi za mapambano hayo kwakutoa taarifa zinazohusiana na rushwa na wahujumu uchumi visiwani Zanzibar.

Aidha Mheshimiwa Makarani ameongeza kuwa rushwa ya muhali ni moja miongoni mwa sababu zinazopelekea kurudisha nyuma mapambano dhidi ya vitendo vya rushwa na uhujumu uchumi, hivyo basi ameiomba jamii kuachana na tabia ya muhali ili kutokomeza vitendo hivyo.

Akiwasilisha mada katika mkutano huo Mwenyekiti wa Klabu ya Waandishi wa Pemba (PPC) Ali Mbarouk Omar amesema waandishi wa habari wana jukumu kubwa la kutoa taarifa dhidi ya vitendo vya rushwa na uhujumu uchumi ili taaluma zao ziweze kuleta tija kwa maslahi ya taifa.

Fat-hia Mussa Said ni mratibu Chama Cha Waandishi wa habari Wanawake Kisiwani Pemba, amesema licha ya kampeni zinazo fanywa na tamwa za kuongeza uelewa kwa jamii juu ya wanawake kugombea nafasi mbali mbali za uongozi lakini bado kuna changamoto kadha wa kadha zinazowakabili wanawake katika kugombea nafasi hizo ikiwemo rushwa ya ngono, mfumo dume, Dini pamoja na mila na desturi.

Nae afisa elimu kutoka Zaeca Yussuf Juma Suleiman amewaomba waandishi hao kuwa wabunifu kwa kutoa taarifa mbali mbali zinazohusiana na maendeleo pamoja na taarifa za rushwa na uhujumu uchumi badala ya kutumia muda mwingi kufanya mahojiano na maafisa kutoka ZAECA.

Ali Massoud Kombo ni mwandishi wa habari kutoka Micheweni Community Radio na UGA TV amehoji kuhusu suala la ZAECA kutokufatilia taarifa za rushwa amabazo zinahusu kiwango kidogo cha fedha jambo ambalo linarudisha nyuma mapambano hayo.

Akitoa ufafanuzi kuhusu madai hayo afisa dhamana kutoka Mamlaka ya Kuzia rushwa na uhujumu uchumi Zanzibar Suleiman Ame Juma amesema madai hayo hayana ukweli wowote kwani zipo kesi kadhaa ambazo ziko mahakamani zinazohusiana na rushwa ya kiwango kidogo cha fedha.

Nao baadhi ya waandishi walioshiriki katika mkutano huo wamesema baadhi ya waandishi wamekuwa na khofu katika utoaji wa taarifa dhidi ya vitendo vya rushwa na uhujumu uchumi kutokana na vitisho wanavyopokea kutoka kwa baadhi ya watuhumiwa wa makosa hayo.

Akiwatoa khofu waandishi wa habari kuhusu suala hilo Mkurugenzi kutoka ZAECA Ahmed Khamis Makarani amewataka waandishi hao kutokuwa na khofu katika kutoa taarifa za rushwa na uhujumu uchumi sambamba na kuwaahidi kuwapatia ulinzi ili kuendelea kuwa salama katika kutekeleza kazi zao.

Mkutano huo uliowakutanisha watendaji wa mamlaka ya kuzuia rushwa na uhujumu uchumi Zanzibar (ZAECA) pamoja waandishi wa habari ni sehemu ya maandalizi ya kuelekea katika kilele cha maadhimisho ya siku ya rushwa duniani yanayofanyika Disemba 9 kila mwaka.

